JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA TATU
MARCHI 2023




## Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Yakabidhi misaada ya kibinadamu kwa Serikali ya Malawi

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.



Tutumie rasilimali zilizotolewa kufanya kazi – Waziri Simbachawene

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. George Simbachawene, amewataka watumishi wa Ofisi hiyo kutumia rasilimali zilizotolewa kufanya kazi kwa bidii na ufanisi.

Mhe.Simbachawene ameyasema hayo mapema leo Jijini Dodoma wakati wa Kikao cha Baraza la Wafanyakazi la Ofisi hiyo kilichokutana kwa lengo la kujadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 pamoja na makisio ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Aliendelea kusema kuwa, Baraza la Wafanyakazi ni jukwaa muhimu sana mahala pa kazi kwani ni kiunganishi kati ya Menejimenti na Watumishi, na alibainisha kuwa, Serikali inazingatia sana suala la Wizara na Taasisi zake kuwa na mabaraza ya wafanyakazi kwani, yanaanzishwa kisheria kwa madhumuni ya kuishauri Serikali katika ngazi za Idara, Taasisi na Wizara ili kuweza kusimamia kazi na rasilimali watu.

Alibainisha kuwa mabaraza haya yana majukumu ya kulinda haki na wajibu wa waajiri na wafanyakazi, kutoa ushauri kuhusu kujenga hali bora za kazi, masilahi ya wafanyakazi na kusimamia haki na ustawi katika sehemu za kazi. Wajibu wa mabaraza haya kama vyombo vya ushauri na usimamizi ni kuhakikisha kuwa waajiri na watumishi wanatambua wajibu na haki zao, pia wanazingatia maadili ya utumishi wao ili kuleta matokeo ya utendaji wa kazi yenye tija, staha na upendo.

Ameshauri menejimenti kupitia baraza hilo la wafanyakazi, kuwa na utaratibu mzuri wa kuwapongeza wafanyakaki wanaotekeleza majumu yao kwa uweledi,"kuna watumishi ambao kufaya kazi kwa weledi na biidi, na kuwahudumia wananchi kwao ni kama sehemu ya ibada." Alifafanua

Aliendelea kusema kuwa Utumishi wa umma wa zama hizi ni watu wenye ueledi,wasomi na wenye cv kubwa,lakini wanashindwa kuuonesha kutokana na mazingira kutokuwa rafiki,aliwaasa watumishi wa ofisi hiyo kufanya kazi ya umma kwa bidii.

"Jukumu kubwa kwa ninyi viongozi ni kuwahudumia wadogo ili waweze kuleta matoke."alisema Mhe. Simbachawene.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi aliwashukuru watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutekeleza majukumu yao na kusimamia shughuli mbali mbali za serikali kwa kujituma na kwa ufanisi mkubwa.



# Dkt. Yonazi ahimiza kasi miradi ya ujenzi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. Jim Yonazi ameridhishwa maendeleo ya miradi ya ujenzi inayosimamiwa na Ofisi hiyo ambapo amesema kukamilika kwake kutawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Dkt. Yonazi ameyasema hayo alipofanya ziara ya kutembelea na kukagua ujenzi wa maeneo yenye miradi ya ujenzi iliyopo chini ya Ofisi hiyo na kuwataka wakandarasi kuongeza juhudi ili majengo hayo yakamilike kwa wakati kama ilivyokusudiwa

Amesema uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa .Dkt. Samia Suluhu Hassan kutekeleza miradi hiyo mikubwa ni kuhakikisha shughuli za Serikali zinafanyika katika mazingira yenye ubora na kuhudumia wananchi kwa weledi.

"Tumefanya ukaguzi wa majengo ya Kituo cha Operesheni ya Maafa, jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, jengo la Idara ya Kupiga Chapa Kisasa na jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) Mtumba na maendeleo ni mazuri," Amesema Dkt. Yonazi.

Pia amewahimiza wakandarasi kuhakikisha wapata vifaa kwa wakati ili ujenzi huo kufanyika ndani ya muda uliopangwa pamoja na wasimamizi kusimamia kikamilifu kuhakikisha majengo hayo yanakuwa na ubora unaotakiwa.

"Tumetoa angalizo kwamba lazima usimamizi uwe mzuri na majengo yakamilike kwa wakati, zipo changamoto mbalimbali kama vifaa lakini tumekubaliana wakandarasi wafuatilie vifaa ili majengo haya yatumike na watumishi wa Serikali na wakae sehemu mmoja kutumikia wananchi kwa pamoja," Ameeleza Katibu Mkuu huyo.

Aidha amewahimiza kuongeza ubunifu wa utendaji kazi hatua itakayosaidia kuhamasisha kazi kufanyika kwa mwamko na ubora zaidi .

Kwa upande wake Mkadiriaji Majenzi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi Mhandisi Saudeni Anania ameishukuru Serikali kwa kuendelea kushirikiana nao huku akisema wanakabiliwa na changamoto ya vifaa vya umaliaziaji ujenzi.



# Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Yakabidhi misaada ya kibinadamu kwa Serikali ya Malawi

Balozi wa Tanzania Nchini Malawi Mhe. Humphrey Polepole ameshiriki katIka zoezi la kukabidhi misaada ya Kibinadamu kutoka Tanzania kwa Serikali ya Malawi ili kusaidia wahanga wa Kimbunga Freddy.

Balozi amekabidhi misaada hiyo ya kibinadamu inayojumuisha Mablanket, Mahema, Unga wa Mahindi kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Malawi Mhe. Nancy Tembo katika Mji wa Blantrey Nchini Malawi Balozi Polepole alibainisha kuwa wa watanzania, na watu wa Malawi ni jamii moja, na Nia ni kuendekeza umoja uliojengwa na waasisi wa Nchi zetu.

" Msaada huu wa kibinadamu utasaidia, katika jitihada za kurejesha matumaini na ustawi kwa ndugu zetu Wananchi wa Malawi", Alisisitiza Balozi Polepole.

Aliongeza kusema kuwa ana imani na wapiganaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania walioenda Nchini Malawi watashirikiana na wenzao Wanajeshi wa Malawi, kuhakikisha kwamba misaada iliyotolewa inawafikia Wahanga wa Kimbunga Freddy.

Aidha, Tanzania imetoa madawa ya binadamu, ambayo yataweza kusaidia kwenye maeneo ambayo vituo vya afya vimeathirika. Hizi zote ni jitihada za kusaidia Nchi ya Malawi katika kurejesha huduma za afya.

"Tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Msaada aliotoa kwa Nchi ya Malawi, kwa uwezeshaji wa fedha na wapiganaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (Wahandisi wa Medani) ambao watasaidia katika kurejesha hali ya miundo mbinu Nchini Malawi," alisema Balozi.



# Meja Jenerali Mbuge “Mikoa Ianzishe timu za wataalam ya kukabiliana na Maafa

Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu Meja Jenerali Charles Mbuge amewataka Wataalam kuanzisha Timu Mtambuka ya Wataalam ya Kukabiliana wa Maafa kila Mkoa ambayo itarahisisha mawasiliano ndani ya Mkoa wakati wa kukabiliana na dhahrura.

Meja Jenerali Mbuge ameyasema hayo wakati akifungua Kikao Kazi cha Kuweka Mkakati wa Kuanzisha Timu ya Wataalam ya Kukabilianana Maafa Mkoa wa Dodoma (Dodoma Mult Agency Emergency Response Team – DoMAERT) kilichofanyika Jijini Dodoma.

Amesema uwepo wa timu hiyo pia itasaidia kuunganisha nguvu kwa wadau waliopo ndani ya Mkoa na kuweza kutumia rasilimali zilizopo kuhakikisha maafa yanakabiliwa na wananchi kuwa katika mazingira salama.

“Nchi yetu imekuwa ikipata maafa mara kwa mara ambayo uratibu wake unahitaji kila Mkoa kuwa na Timu Mtambuka ya Wataalam ya Kukabiliana wa Maafa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi ya Maafa Na. 6 ya mwaka 2022 na kanuni zake hivyo uundwaji wa timu hizo ni muhimu kwa usalama wa wananchi na mali zao,” Amesema Meja Jenerali Mbuge.

Pia Mkurugenzi huyo amewasisitiza washiriki kupitia kikao kazi hicho kuhakikisha kila mmoja kwa nafasi yake anafahamu jukumu lake na kulitekeleza kikamilifu pamoja na tayari kwa ajili ya kukabiliana na maafa ndani ya Mkoa.

Katika hatua nyingine ameeleza Meja Jenerali Mbuge kwamba Idara ya Menejimeti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kuchukua hatua za kupunguza madhara kwa kuhakikisha usimamizi na uratibu wa maafa na huduma za dharura zinatolewa kwa wakati kwa kuzingatia mipango, miongozo na mikakati ya kitaifa na kisekta.

"Idara ya Menejimenti ya Maafa kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Na. 6 ya mwaka 2022 inaratibu na kusimamia masuala ya maafa nchini,"Amebainisha Mkurugenzi huyo.

Aidha Mkurugenzi huyo akawahimiza wananchi kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wa maendeleo ili kuhakikisha malengo ya mapambano dhidi ya maafa yanafaikiwa kama iliyokusudiwa.



# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Yapokea na kujadili taarifa ya muundo wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA)

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imepokea na kujadili muundo wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) nchini.

Kikao hicho kilichofanyika Jijini Dodoma kimeongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Joseph Mhagama na kuhudhuriwa na wajumbe wa Kamati hiyo pamoja na wadau mbalimbali.



# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria, yatembelea miradi ya ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Kiwanda cha Uchapaji wa Nyaraka za Serikali

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria imeonesha kuridhishwa na hatua ya ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji wa Nyaraka za Serikali Mjini Dodoma.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria Mhe. Joseph Mhagama, katika ziara ambayo ililenga kujionea kile ambacho kimepangwa kwenye bajeti ya Serikali na kuangalia hatua zilizopigwa, changamoto zilizojitokeza na namna ya utatuzi wake.

"Ziara hii imetuwezesha kupata uhalisia wa hali jinsi ilivyo, ili iweze kutusaidia wakati wa kupanga bajeti, tuwe na uhalisia wa utekelezaji miradi" alisema.

Akizungumzia kuhusu Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Mhe. Mhagama amesema upo muhimu wa Idara hiyo kuwa na mifumo rasmi ya kujisimamia bajeti yake yenyewe (kama wakala) ili isaidie idara hiyo iweze kuingia katika soko shindani.

Aliongeza kusema Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ikiweza kujisimamia katika bajeti yake, itasaidia kuongeza Makusanyo mengi ambayo yanategemewa kutoka katika Idara hiyo.

Tunachangamoto kubwa sana katika utengenezaji wa nembo ya Taifa, "lazima tuwe na Mamlaka moja ya kutengeneza nembo ya Taifa na watu wengine wote waipate kupitia katika Ofisi ya Mpiga Chapa wa Serikali, "alisema Mhe. Mhagama.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amesema anakubaliana na maelekezo ya Kamati. Wizara itatoa taarifa mbele ya Kamati hatua iliyofikia katika kuandaa mabadiliko ya sheria ili kuwezesha Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa wakala.

Naye Mhe. Ahmed Ngwali Mjumbe wa Kamati, ameshauri Idara ya Mpiga Chapa Mkuu Wa serikali Kufanyia kazi mapendekezo ya Kamati mapema ili iweze kubadilishwa na kuwa wakala.

Awali Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Bwn. George Lugome amesema Utakapokamilika mradi wa Kiwanda cha Uchapaji wa Nyaraka za Serikali itasaidia kuimarika kwa utunzaji wa kumbukumbu ikiwa ni sambamba na kuongeza ajira na kuwa sehemu ya mafunzo kwa watu wanasomea maswala ya uchapishaji.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.





KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz